

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA THELATHINI NA SABA**

**03 JUNI, 2022**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA SABA – TAREHE 03 JUNI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

#### **WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

#### **WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

#### **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

### III. MASWALI:

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

#### 325. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza kutenga fedha za dharura kwa ajili ya barabara.

#### 326. MHESHIMIWA STELLA ALEX IKUPA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni Halmashauri na Manispaa ngapi nchini zinatekeleza ununuzi na ugawaji wa mafuta ya ngozi kwa Watu wenye ulemavu wa ngozi.

**327. MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY  
MAGANGA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Mradi wa barabara wa Km 96 unaofadhiliwa na Benki ya Dunia utafika Mbogwe.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO  
WA AFRIKA MASHARIKI:**

**328. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL  
ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua Ubalozi wa Tanzania nchini Pakistan.

**WIZARA YA KILIMO:**

**329. MHESHIMIWA EMMANUEL PETER  
CHEREHANI (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha majadiliano na Kampuni ya Tanzania *Leaf Tobacco* ili iweze kurudi nchini kuendelea kununua Tumbaku.

**330. MHESHIMIWA EMMANUEL MAGENI KASALALI (SUMVE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni kwa nini Serikali isiyaondoe Mazao ya Choroko na Dengu kwenye utaratibu wa Stakabadhi Ghalani.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**331. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMED KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzijenga kwa kiwango cha lami barabara zilizokwisha fanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO  
YA MAKAZI:**

**332. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA  
(SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi,  
Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, nyumba bora ya kuishi inatakiwa kuwa na  
sifa zipi na ni kwa nini Serikali haiweki ruzuku  
kwenye vifaa vya ujenzi.

**WIZARA YA MAJI:**

**333. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itaipatia Ruzuku Bodi ya Maji  
ya KAVIWASU kwa kuwa imekuwa  
ikiendeshwa kwa gharama za Wananchi.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**334. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini ujenzi wa Chuo cha VETA Burugo – Nyakato katika Jimbo la Bukoba Vijijini utakamilika.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**DODOMA  
03 JUNI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**